**EUROPEAN UNION**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**05/12/2013**

# Mpango mpya wa Umoja wa Ulaya (EU) kusaidia kupunguza vifo haramu vya tembo na viumbe vingine vilivyo hatarini kutoweka katika nchi zinazoendelea.

Hivi karibuni ongezeko la uwindaji haramu na biashara haramu ya viumbe pori limevunja rekodi, huku nchi zenye tembo, nchi za mpito na nchi watumiaji walikutana katika Mkutano wa Tembo Africa, uliofanyika Gaborone, Botswana mapema wiki hii.

Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) imeamua kuunga mkono mpango wa kuboresha ulinzi wa tembo, nyani na vifaru, Afrika, pamoja na aina nyingine ya viumbe adimu katika Karibiani na Pasifiki. Hatua hii itaimarisha ufuatiliaji wa idadi ya wanyama na vitendo vya ujangili, kusaidia kuboresha utekelezaji wa sheria katika mapambano dhidi ya uwindaji haramu kwa njia ya mafunzo na msaada wa uendeshaji, na kuanzisha mfumo wa dharura ikitokea ongezeko la ghafla la uwindaji na biashara haramu.

Kamishna wa Ulaya wa Maendeleo, Andris Piebalgs, ameeleza kuwa *"Uwindaji haramu wa viumbe hatarishwa hivi sasa ni moja ya tishio kubwa kwa wanyamapori katika nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki. Unahusisha mitandao ya kijangili yenye silaha za uwezo mkubwa, na hivyo kuhatarisha hali ya usalama matokeo yake hudhoofisha maendeleo. Zinahitajika njia madhubuti kwa lengo la kukabiliana na matisho dhidi ya viumbe hai na usalama katika maeneo hayo matatu. "*

Kamishna wa Ulaya – Mazingira, Janez Potocnik, amesema, *" Mpango huu mpya unaonyesha kwamba Umoja wa Ulaya (EU), kwa kushirikiana na nchi za ACP, uko tayari kuimarisha jitihada zake za kupambana na biashara haramu ya uwindaji wanyamapori na kupunguza athari zake kubwa katika kuhatarisha uwepo wa viumbe hai. Kwa kiasi kikubwa ninakaribisha malengo yanayozingatia utekelezaji bora wa sheria za Mkataba wa Biashara ya Kimataifa kwa Viumbe vilivyo Hatarini (CITES), ambayo yatasaidia nchi kuimarisha uwezo wao katika eneo hilo. Hata hivyo, kutokana na ongezeko kubwa la soko la bidhaa za uwindaji haramu wa wanyamapori, na ukweli kwamba uhalifu wa uwindaji wanyamapori pia kuwa tishio kubwa kwa usalama, utulivu wa kisiasa, maliasili na utawala wa sheria, Umoja wa Ulaya unahitaji kufikiria kama mbinu zake za sasa zinajitosheleza katika kukabiliana na wingi wa sura mbalimbali zinajitokeza katika swala hili."*

**For more information, please contact: Mr. Tom Vens**, Head of Political Press and Information Section
Delegation of the European Union to Tanzania
**Email**: Tom.VENS@eeas.europa.eu
**Direct Line: +255 22 2164503**
**Website**: http://eeas.europa.eu/delegations/tanzania/index_en.htm
**Facebook**: https://www.facebook.com/EuropeanUnionTanzania

Mradi huu mpya wa "Kupunguza Mauaji haramu ya Tembo na viumbe wengine walio Hatarini" (MIKES) ni mwendelezo wa miradi kama hiyo ambayo imekuwepo tangu mwaka 2001: umefanikiwa kuandaa takwimu zinazo onyesha ongezeko la kutisha la vitendo vya ujangili dhidi ya tembo na kuonyesha haja kubwa ya kuchukua hatua dhidi ya kuenea kwa biashara haramu ya kimataifa ya pembe za ndovu. Kwa mujibu wa takwimu za mradi huo, mwaka 2012 karibu tembo 22,000 waliuawa kinyume cha sheria katika bara la Afrika. Takwimu hizi zinaonyesha kasi ya idadi hiyo ni kubwa ukilinganisha na kasi ya idadi ya tembo waliopo inavyokua, na hivyo kupendekeza kuwa idadi ya tembo kwa ujumla inapungua. Biashara haramu ya pembe pia inashika kasi: mwaka 2011 ulishuhudia rekodi kubwa ya kukamatwa kwa tani 35 za pembe.

Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifiki zinjivunia viwango vya juu vya uwepo wa viumbe hai na baadhi ya viumbe hivi ni adimu duniani, kama vile vifaru, nyani wa kubwa na kasa wa baharini. Mradi mpya wa MIKE utaboresha mfumo wa ufuatiliaji viumbe hai na hatari zozote kwao na kupanua wigo huo kutoka tembo na kujumuisha viumbe vingine adimu. Ili kupambana na mauaji haramu, miongoni mwa mambo mengine, mradi utatoa mafunzo ya utekelezaji wa sheria, msaada wa kiufundi kwa ajili ya kuanzisha mifumo ya doria, msaada wa utekelezaji utakaozingatia mahitaji halisi.

---

**Historia fupi**

Mradi wa "Kupunguza Mauaji haramu ya Tembo na viumbe wengine walio Hatarini" (MIKES) unafadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya wa awamu ya 10 wenye kiasi cha € 12,300,000 na kuendeshwa kwanzia mwaka 2014-2018. Utatekelezwa na Mkataba wa Biashara ya Kimataifa wa Viumbe vilivyo Hatarini Kutoweka aina ya Fauna na Flora pori (CITES) kwa kushirikiana na majimbo 31 ya Afrika yaliyo na tembo pamoja na katika baadhi ya maeneo ya hifadhi katika ukanda wa Karibiani na Pasifiki.

**For more information, please contact: Mr. Tom Vens**, Head of Political Press and Information Section
Delegation of the European Union to Tanzania
**Email**: Tom.VENS@eeas.europa.eu
**Direct Line: +255 22 2164503**
**Website**: http://eeas.europa.eu/delegations/tanzania/index_en.htm
**Facebook**: https://www.facebook.com/EuropeanUnionTanzania